**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. UDC/L.40/08/19** **01 Machi 2021**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (READVERTISED)

### MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA (NAFASI 01).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu anawatangazia nafasi za kazi watanzania waishio katika maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, wenye sifa, na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, kutuma maombi ya nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira.

### SIFA ZA MWOMBAJI.

1. Awe raia wa Tanzania anayeishi katika maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.
2. Awe amestaafu Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Sheria.
3. Awe hajawahi kutiwa hatihani kwa makosa ya jinai.
4. Awe na umri wa kuanzia miaka 55 na kuendelea.
5. Awe na Elimu ya Shahada kutoka vyuo vya Elimu ya Juu vinavyotambuliwa na Serikali katika moja wapo ya fani za Utawala, Usimamizi wa Rasilimaliwatu, au Sheria.

### KAZI/ MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA.

1. Kuongoza vikao vya Bodi ya Ajira katika ngazi ya Halmashauri.

### VIGEZO NA MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania na mwenye umri wa kuanzia miaka 55.
2. Mwombaji aambatanishe wasifu binafsi (Curriculum Vitae) yenye mawasiliano ya uhakika kama vile anuani, namba za simu, barua pepe, pamoja na wadhamini watatu wa kuaminika (Referees).
3. Maombi yote yaambatanishwe na cheti cha kuzaliwa, cheti cha kidato cha nne au cha sita, na vyeti vya taaluma, na ni lazima view vimethibitishwa na Hakimu, au Wakili anayetambuliwa na Serikali.
4. Maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

5. Maombi yote yaandikwe kwa mkono na yaambatanishwe na picha moja ya 'passport size' ya hivi karibuni (iandikwe jina kwa nyuma).
6. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili hayatafikiriwa.
7. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 14 Machi 2021 saa 9:30 Alasiri.

Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu,
S.L.P. 50,
**KAHAMA.**

Michael A. Matomora
**MKURUGENZI MTENDAJI**

MKURUGENZI MTENDAJI (W) HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU
01 MAR 2021

**Nakala:** Katibu Tawala (M),
S.L.P 320,
**SHINYANGA.**

Katibu Tawala (W),
S.L.P 01,
**KAHAMA.**

Mbao zote za Matangazo,
Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Msalala, na Manispaa ya Kahama.
**KAHAMA.**